

**PENDO HILI PENDO GANI NA KWANGU LANITAKANI?**

1. Pendo limenisakama, moyoni limegandama.  
Kila nikilitazama, siachi kuliandama.  
Fikirani limenikwama, mwili wanizizima.  
Pendo hili pendo gani, kwangu lanitakani?
2. Pendo haliniachi, kutwa liko mlangoni.  
Hauchi wala hakuchi, pendo li barabarani.  
Uzuriwe hafichi, heshi kutia vimini.  
Pendo hili pendo gani, kwangu lanitakani?
3. Mwendowe wa maringo, hatua za kuchagua.  
Huyumba yake shingo, machowe kurembua.  
Hutingishika maungo, vile anavyotembea.  
Pendo hili pendo gani, kwangu lanitakani?
5. Sikiliza asemapo, sauti yake kinanda.  
Mithili ya upepo, pumzi inavyopanda.  
Utapandisha pepo, mwingine hutampenda.  
Pendo hili pendo gani, kwangu lanitakani?
6. Sasa ngoja akicheka, uyaone yake meno.  
Jinsi yalivyopangika, vigumu kutia neno.  
Meupe yametakasika, sifaze zaidi mno.  
Pendo hili pendo gani, kwangu lanitakani?
7. Tazama kichwa chake, mviringo chogole,  
Nyeusi nywele zake, ajabu vyake vidole.  
Na hasa rangi yake, pamwe na wake upole.  
Pendo hili pendo gani, kwangu lanitakani?
8. Nawatafuta waganga, pendo waniepushe.  
Nimefika Sumbawanga, janga hili wanivushe.  
Hawakuweza wa Tanga, naomba mnikumbushe.  
Pendo hili pendo gani, kwangu lanitakani?

*Yusuf Kalala. Washington, DC  
August, 2002*